TOLEO MAALUM
# HALMASHAURI
YA JIJI LA DODOMA

Dodoma jiji | Dodomajiji_ Tz | Dodomajiji Tz | Dodoma City Tv

## Pongezi nyingi kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa tena kutumikia miaka mitano ya kipindi cha pili



# Jiji la Dodoma
## latoa Milioni 545 kwa wajasiliamali


HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetoa mikopo yenye thamani ya zaidi ya shilingi 545,000,000 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2020/2021 ili kuviinua vikundi hivyo kiuchumi.

Hayo yalikuwa kwenye taarifa ya utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dkt. Binilith Mahenge, taarifa iliyosomwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma Joseph Mafuru katika halfa ya kukabidhi mikopo hiyo iliyofanyika katika bustani ya Nyerere 'square' jana.

Mkurugenzi Mafuru alisema kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Halmashauri ya Jiji la Dodoma imetenga jumla ya shilingi 2,262,708,770 kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. "Katika robo ya kwanza ya Julai-Septemba, 2020, Halmashauri imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 545,000,000. Vikundi saba vya wanawake vimepewa shilingi 125,000,000, vikundi viwili vya




Jiji la Dodoma Kubadilika kimazingira
Utekelezaji wa Miradi
Fulsa za uwekezaji
Habari Matangazo



## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

**Inatoa pongezi nyingi kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli , Makamu wa Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa tena kuitumikia miaka mitano ya kipindi cha pili**



# Rais Magufuli aapishwa, aahidi makubwa, Jiji la Dodoma lazizima

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Magufuli aahidi kuendelea kukuza uchumi na kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana, muda mfupi baada ya kula kiapo (pichani) kwa nafasi ya urais tukio lililofanyika katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma leo.

Rais, Dkt Mafuguli amesema kuwa jukumu alilonalo ni kukuza uchumi wa Watanzania na kukabiliana na ukosefu wa ajira kwa vijana. "Serikali ninayoiongoza itazidisha mapambana dhidi ya rushwa, wizi na ubadhirifu wa mali ya umma" alisema Dkt. Magufuli.

Aidha, ameahidi kujenga uwanja mkubwa wa kisasa wa michezo jijini Dodoma. "Shukrani sana wana Dodoma kwa kuhudhuria kwa wingi kwenye tukio hili. Watu wameanza kuingia uwanjani usiku, nawashukuru kwa heshima hii kubwa mliyonipa na imedhihirisha kuwa Dodoma ndiyo Makao Makuu ya nchi. Serikali itakayoanza leo, kitu cha kwanza ni kujenga uwanja mkubwa wa michezo hapa Dodoma ili sherehe zijazo watu wote wa Dodoma wawe ndani ya uwanja washerehekee vizuri" alisema Rais, Dkt. Magufuli.

Amesema kuwa Chama Cha Mapinduzi kimepata ushindi mkubwa kutokana na baraka za wana Dodoma kwa sababu uzinduzi na kilele cha kampeni



*RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Magufuli akila kiapo kushika nafasi hiyo kwa miaka mingine mitano uwanja wa Jamhuri Dodoma*

za uchaguzi mkuu zilifanyika Jijini Dodoma. "Yote tuliyoahidi tutayashughulikia ikiwemo ujenzi wa barabara ya mzunguko, sababu msongamano umeanza kuonekana Dodoma" aliongeza Rais huyo.

Akitoa salamu kwa niaba ya wananchi wa Jamhuri ya Comoro, Rais wa nchi hiyo, Azali Assoumani alimuomba Mungu kumsaidia sana Rais, Dkt. Magufuli kutekeleza kazi aliyopewa na watanzania kwa ufanisi.

"Nachukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Tanzania kukamilisha salama mchakato wa uchaguzi, nawashukuru kwa uwepo wao hapa. Tunashukuru kila tunapokuja Tanzania mimi na ujumbe wangu tunapokelewa vizuri na kujisikia tupo nyumbani" alisema Rais Assoumani.



*Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan akila kiapo kushika nafasi hiyo kwa miaka mingine mitano uwanja wa Jamhuri Dodoma*

Nae, Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa alisema "naleta salamu nyingi kutoka kwa wananchi wa Zimbabwe. Tunamshukuru Rais, Dkt. Magufuli alifanya ziara nchini Zimbabwe. Na wakati wa ukame mkali, Rais Dkt. Magufuli alitupatia msaada wa mahindi kwa Wazimbabwe. Huyu ni kiongozi mzalendo katika ukanda huu".

Wakati huohuo, Mwanazuoni na Mhadhiri wa Sheria kutoka Kenya, Prof. Patrick Loch Otieno Lumumba kupitia televisheni ya TBC amempongeza Rais, Dkt. Magufuli na CCM kwa ushindi mkubwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Prof. Lumumba ametoa tahadhari kuwa makini na wafadhili wavurugaji nchi za kiafrika. "Katika nchi za kiafrika, tuwe wepesi kujiepusha na wafadhili wenye lengo la kuvuruga nchi za Afrika. Tatizo la nchi za Afrika ni kutotofautisha upinzani na ubabaishaji. Tuhakikishe tunaendesha siasa ambazo zinalinda usalama wetu" amesema Prof. Lumumba kwa msisitizo.

Rais, Dkt. John Pombe Magufuli ameapishwa leo katika sherehe za aina yake zilizofanyika kwa mara ya kwanza Jijini Dodoma katika uwanja wa Jamhuri tangu Dodoma kupata hadhi ya Jiji na kuwa Makao Makuu ya nchi.

# MATANGAZO!

## MNADA WA KUPANGISHA BUSTANI YA MAPUMZIKO CHINANGALI RECREATIONAL PARK

**Tarehe 21 Novemba, 2020  Saa 3:00 Asubuhi**



*Bustani hiyo ni mradi mpya na ni eneo linalovutia sana kwa mapumziko na burudani mbalimbali ikiwemo uwanja wa kisasa wa mpira wa kikapu, Uwanja wa Tenisi, Mpira wa Wavu, mabwawa ya kuongelea wakubwa na Watoto, eneo la michezo ya watoto, jukwaa la sanaa na GYM. Pia kuna maeneo ya kuuzia vyakula na vinywaji pamoja na eneo kubwa la maenegesho ya Magari.*

## Siku ya mnanda kila mshiriki atatakiwa;

- Kujisajili kwenye regista.
- Kulipa dhamana ya fedha taslimu Tsh. 2,000,000/ (Millioni mbili) ambayo itarudishwa mara baada ya mnada kwa mshiriki ambaye hatafanikiwa.
- Mshindi atalipa asilimia 25 ya kodi ya pango ya kipindi cha miezi mitatu siku ya mnada na kumalizia asilimia 75 kabla ya kuanza kuendesha bustani hiyo.
- Aidha, atawajibika kulipa kodi zote za Serikali kwa mujibu wa Sheria za nchi

**Kwa maelezo zaidi piga simu namba 0622 020211**

## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

Inatoa Pongezi Nyingi kwa Mhe. Kasimu Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Tanzania kwa kuchaguliwa tena kiutumikia miaka mitano ya awamu ya pili na kuidhinishwa na bunge kuwa waziri mkuu wa jumhuri ya muungano wa Tanzania

#HAPAKAZITU



# Rasmi, Kassim Majaliwa Waziri Mkuu tena!



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassimu Mjaliwa Akitoa shuklani katikabunge la 12 baada ya kumpitisha kwa asilimia 100% kuwa waziri mkuu*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli leo amempendekeza Mbunge wa Ruangwa Mhe. Kassim Majaliwa kuwa Waziri Mkuu wa kipindi cha pili cha Serikali ya awamu ya tano mbele ya Bunge.

Wabunge wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakapata nafasi ya kupiga kura kuthibitisha uteuzi huo uliokuwa ukisubiriwa kwa hamu kubwa.

Akitangaza matokeo ya kura zilizopigwa na Wabunge, Spika wa Bunge Job Ndugai amesema Majaliwa amepigiwa kura 350 na hakuna kura iliyoharibika hivyo amepitishwa kwa asimilia 100%.

Akiongea kwa unyenyekevu, Mhe. Kassim Majaliwa alimesema "Jambo hili si dogo, namshukuru sana (Dkt. Magufuli) kwa imani yake kubwa aliyonayo juu yangu na kuendelea kuniamini kwamba naweza kufanya niliyofanya katika kipindi cha miaka mitano na zaidi katika kipindi kingine kijacho,

Niendelee kumhakikishia kwamba matamanio yake yaliyompelekea kutoa jina hilo kulileta mbele ya bunge hili tukufu ambayo anaamini na wabunge wenzangu kwa namna ambavyo mmepiga kura nyingine ni namna tosha mheshimiwa rais ameleta jina ambalo mnaamini nitamsaidia kazi, nami niwahakikishie nitafanya hivyo" amesema Majaliwa kwa kujiamini.



# Hotuba ya Uzinduzi wa Bunge, JPM aitaja Dodoma sekta ya barabara



***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania  Mhe.Dkt.John Pombe Mgufuri akitoa hutuba ya ufunguzi wa Bunge la 12 Jiji Dodoma***

"...hapa Dodoma tumepanga kujenga barabara ya mzunguko ya njia nne yenye urefu wa kilometa 110 ambapo makandarasi wawili tayari wameshapatikana na ujenzi utaanza hivi karibuni"

Hayo yamesemwa na Rais Dkt. John Magufuli jana ikiwa na sehemu ya hotuba yake yenye kuonesha mwelekeo wa utekelezaji wa Serikali ya awamu ya tano katika kipindi chake cha pili.

" Tutakamilisha ujenzi wa kilometa 2,500 za lami na kuanza ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilometa 6,006 najua Wabunge wengi mmetoa ahadi za barabara za lami kwenye maeneo yenu, Ili hatimaye tuweze kufikia lengo letu la kuunganisha Mikoa na Wilaya kwa barabara za lami, barabara hizo zimetajwa kwenye ilani yetu ya Uchaguzi na nyingine zinatokana na ahadi tulizozitoa katika kipindi cha Kampeni." alisema Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Tumepanga pia kukamilisha ujenzi wa madaraja saba  na kuanza madaraja mengine 14, ikiwemo daraja la Busisi, Wami na Pangani " Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Zaidi ya hapo tutaendelea kushughulikia tatizo la msongamano wa magari kwenye Miji na Majiji yetu hususan Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na hapa Dodoma ambapo tumepanga kujenga barabara ya mzunguko ya njia nne yenye urefu wa kilometa 110 ambapo Makandarasi wawili tayari wamekwishapatikana na ujenzi utaanza hivi karibuni" alifafanua zaidi Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika hotuba yake hiyo iliyokuwa ikisubiriwa kwa hamu kubwa na wabunge pamoja na wananchi.

# Jiji la Dodoma latoa Milioni 545 kwa wajasiliamali




*Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma Joseph Mafuru akisoma taarifa ya utoaji wa mikopo katika vikundi Jijini hapa katika tafrija ya utoaji mikopo Mgeni rasmi akiwa ni Mkuu wa Mkoa Dkt Binilith Mahenge Viwanja vya Nyeresquare Mjini*

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetoa mikopo yenye thamani ya zaidi ya shilingi 545,000,000 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2020/2021 ili kuviinua vikundi hivyo kiuchumi.

Hayo yalikuwa kwenye taarifa ya utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dkt. Binilith Mahenge, taarifa iliyosomwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma Joseph Mafuru katika halfa ya kukabidhi mikopo hiyo iliyofanyika katika bustani ya Nyerere 'square' jana.

Mkurugenzi Mafuru alisema kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Halmashauri ya Jiji la Dodoma imetenga jumla ya shilingi 2,262,708,770 kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. "Katika robo ya kwanza Julai-Septemba, 2020, Halmashauri imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 545,000,000. Vikundi saba vya wanawake vimepewa shilingi 125,000,000, vikundi viwili vya vijana vimepewa shilingi 378,000,000 na vikundi vitano vya watu wenye ulemavu shilingi 42,000,000. Vikundi hivyo vimekopeshwa ili kutekeleza miradi ya usafirishaji na kupewa bajaji na bodaboda, ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, ujenzi wa machinjia ya kuku, utengenezaji wa bidhaa za ngozi, saluni na ushonaji" alisema Mafuru.

Akioelezea historia ya mikopo hiyo, alisema kuwa Halmashauri ilianza kutoa mikopo kwa makundi maalum mwaka wa fedha 2015/2016. "Kuanzia mwaka 2015/2016 hadi mwaka 2019/2020, mikopo iliyotolewa kwa makundi hayo ni shilingi 5,292,829,899. Vikundi 812 vya wanawake vimenufaika na shilingi 3,254,962,583, vikundi 425 vya vijana vimenufaika na shilingi 1,856,537,316 na vikundi 30 vya watu wenye ulemavu vimenufaika na shilingi 181,330,000" alisema mkurugenzi huyo.

Kuhusu ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo hiyo, aliutaja kuwa unaendelea vizuri. "Hadi kufikia mwezi Septemba, 2020 kati ya shilingi 5,292,829,899 zilizokopeshwa, shilingi 2,526,769,984 zimerejeshwa na kiasi kilichobaki ufuatiliaji unaendelea" alisema Mafuru.

Halmashauri ya Jiji la Dodoma imetoa mikopo ya bodaboda 46, bajaji 20 na guta moja kwa vikundi vya vijana zenye thamani ya shilingi milioni 378 kati ya mikopo ya shilingi milioni 545 iliyopokesha makundi maalum robo ya kwanza Julai-Septemba, 2020.

## Kupitia Utoaji wa Mkopo wa Milioni 545 kwa wajasiliamali

***Halmashauri ya Jiji la Dodoma imetoa mikopo ya bodaboda 46, bajaji 20 na guta moja kwa vikundi vya vijana zenye thamani ya shilingi milioni 378 kati ya mikopo ya shilingi milioni 545 iliyopokesha makundi maalum robo ya kwanza Julai-Septemba, 2020.***







# Jiji Dodoma lapongezwa kwa kuunga mkono juhudi za JPM




*Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dkt. Binilith Mahenge (mwenye suti katikati) akikabidhi mfano wa hundi ya shilingi Milioni 545 kwa vikundi vya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu kwenye hafla iliyofanyika kwenye uwanja wa Nyerere Square Jijini Dodoma, kulia kwa Mkuu wa Mkoa ni Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma Joseph Mafuru na kushoto kwake ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma Makuka Kessy, kushoto kabisa ni Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Vijana wa Jiji la Dodoma Sharifa Nabalang'anya na wengine ni miongozi mwa wanufaika wa mikopo hiyo.*

### *Halmashauri ya Jiji la Dodoma imeshatoa zaidi ya Sh. Bilioni 5 kwa wajasiliamali - Mkurugenzi Mafuru*
### *Tunaishukuru Serikali ya awamu ya tano kuifanya mikopo hii kuwa kisheria - Mkuu wa Idara Sharifa*

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imepongezwa kwa kuunga mkono juhudi za Rais Dkt. John Magufuli za washirikisha wananchi katika kujenga uchumi kwa kutoa mikopo ya thamani ya shilingi 545,000,000 kutoka mapato yake ya ndani katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2020/2021.

Pongezi hizo zimetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Binilith Mahenge katika halfa fupi ya kukabidhi mikopo ya asilimia 10 kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri kwa vikundi iliyofanyika katika uwanja wa Nyerere 'Square' jijini hapa.

Dkt. Mahenge alisema "leo tunashuhudia Rais, Dkt. John Magufuli akiwashirikisha wananchi na makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika shughuli za kiuchumi. Baada ya utaratibu huu wa mikopo ya asilimia 10 utekelezaji wake kusuasua, serikali ya awamu ya tano ilipoingia madarakani ikatunga sheria. Sheria hii imerahisisha utekelezaji wake. Leo kijana anayekabidhiwa bodaboda anakuwa ametatuliwa changamoto ya usafiri, nae kushiriki katika kutatua changamoto za watu wengine kwa kuwasafirisha. Hivyo kuchochea maendeleo na ukuaji wa uchumi".

Alisema kuwa serikali na makao makuu ya nchi kuhamishiwa Dodoma, kumelifanya Jiji la Dodoma kukua kiuchumi. "Ndugu zangu, matunda na makao makuu ya nchi kuhamia Dodoma, Jiji la Dodoma ndiyo Halmashauri pekee inayotenga na kukopesha fedha nyingi kwa wakundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Haya ni matokea ya serikali kuhamia Dodoma na utendaji kazi nzuri wa Jiji la Dodoma" alisema Dkt. Mahenge.

Alisema kuwa leo atakabidhi bajaji na bodaboda kwa makundi hayo, na kuwataka kuvitunza. "Ombi langu kwenu mnaopokea vifaa hivi au hundi, hii ni fursa kubwa kwenu hakikisheni mnavitunza ili viwaletee maendeleo yaliyokusudiwa" alisema Dkt. Mahenge.

Akiwasilisha taarifa ya utoaji mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru alisema kuwa Halmashauri yake imetoa zaidi ya shilingi bilioni tano kuvikopesha vikundi. "Kuanzia mwaka 2015/2016 hadi 2019/2020, mikopo iliyotolewa kwa makundi hayo ni shilingi 5,292,829,899. Vikundi 812 vya wanawake vimenufaika na shilingi 3,254,962,583, vikundi 425 vya vijana vimenufaika na shilingi 1,856,537,316 na vikundi 30 vya watu wenye ulemavu vimenufaika na shilingi 181,330,000" alisema Mafuru.

Jumla ya vikundi vyote vilivyopata mikopo ni 1,267 vikiwa na wanavikundi 12,670, aliongeza.

Akiongelea ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo hiyo, alisema kuwa unaendelea vizuri. "Hadi kufikia mwezi Septemba, 2020 kati ya shilingi 5,292,829,899 zilizokopeshwa, shilingi 2,526,769,984 zimerejeshwa na kiasi kilichobaki ufuatiliaji unaendelea" alisema Mafuru.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Halmashauri ya Jiji la Dodoma imetenga jumla ya shilingi 2,262,708,770 kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. "Katika robo ya kwanza Julai-Septemba, 2020, Halmashauri imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 545,000,000. Vikundi saba vya wanawake shilingi 125,000,000, vikundi viwili vya vijana shilingi 378,000,000 na watu wenye ulemavu shilingi 42,000,000. Vikundi hivyo, vimekopeshwa ili kutekeleza miradi ya usafirishaji kwa njia ya bodaboda na bajaji, ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, ujenzi wa machinjio ya kuku, utengenezaji wa bidhaa za Ngozi, saluni na ushonaji" alisema Mkurugenzi huyo.

Kwa upande wake Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Vijana Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalang'anya alimshukuru Rais kwa kuifanya mikopo hiyo kuwa kisheria. "Kabla ya serikali ya awamu ya tano, mikopo hii haikuwa kisheria hivyo utekelezaji wake ulikuwa unasuasua, baada ya serikali hii kuingia madarakani ilitunga sheria na kuifanya mikopo kuwa kisheria. Awali mikopo hii ilikuwa kwa ajili ya makundi mawili, wanawake na vijana, lakini serikali hii ilipoingia madarakani imeongeza kundi la watu wenye ulemavu. Wanawake asilimia nne, vijana asilimia nne na watu wenye ulemavu asilimia mbili" alisema Nabalang'anya.

Nae mnufaika wa mikopo hiyo, Mariam Ally kutoka kikundi cha Muwakiki kilichopo Kata ya Tambukareli jijini hapa alishukuru kwa niaba ya vikundi vyote. "Shukrani kwa niaba ya vikundi vyote kwa Jiji la Dodoma, tunashukuru sana kwa uwepo wa mikopo isiyokuwa na riba. Tunamshukuru sana Rais, Dkt. John Magufuli na tunaomba aendelee kuwanufaisha wengine, tunaushukuru uongozi wa Jiji la Dodoma kutusimamia tumepata mikopo na baadhi tumerudisha mikopo hiyo" alisema Ally.

# Dodoma Jiji FC yaipapasa Ruvu Shooting



*Kikosi cha kwanza cha Dodoma Jiji Fc Inayoshiriki Ligi kuu Tanzania bara*

TIMU ya Dodoma Jiji FC leo imedhihirisha ubabe wake katika dimba lake la nyumbani Jamhuri Jijini Dodoma baada ya 'kuipapasa' timu ya Ruvu shooting kwa kuifunga magori 2 - 0.

Mchezo ulianza kwa kila timu kujitahidi kusoma mbinu za mpinzani wake, iliwachukua Dodoma Jiji dakika 30 kuandikisha goli lao la kuongoza kupitia kwa kiungo mshambuliaji Cleophas Mkandala aliyetumia vema makosa ya Golikipa wa Ruvu Bidiyu Abdallah kupiga vibaya mpira ambao ulimfikia mfungaji aliyefunga goli la kiufundi akiupitisha mpira juu ya wachezaji na kujaa wavuni.

Dodoma Jiji ilijipatia goli la pili dakika ya 39 lililofungwa na Jamal Mtegeta akipokea pasi murua kutoka kwa Cleophas Mkandala.

Ushindi wa leo kwa Dodoma Jiji FC umeifanya ifikishe pointi 10 ikisogea kutoka nafasi ya sita hadi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu ya Vodacom baada ya mechi moja ya leo.

Kikosi cha Dodoma Jiji FC leo kiliwakilishwa na Aron Kalambo, Steven Mganga, Jukumu Kibanda, Mbwana Kibacha (Nahodha), Augustino Samson, Rajabu Mgalula, Dickson Ambundo, Cleophace Mkandala, Anuary Jabiri, Khamis Mcha na Jamal Mtegeta. Akiba: Mseja, Wawa, Kapona, Hoza, Kanyoro, Mapunda na Karihe.

# Tanzania U-17 wanawake watwaa ubingwa wa COSAFA



Timu ya Taifa ya soka ya wanawake ya Tanzania ya wachezaji wenye umri chini ya miaka 17 (U-17) 'Tanzanite Queens' imeibuka bingwa wa mashindano ya soka ya wanawake ya Nchi za Kusini mwa bara la Afrika (COSAFA) baada ya kuifunga timu ngumu ya Taifa ya Zambia 4-3 kwa mikwaju ya penalti.

Timu ya wanawake ya Tanzania (U-17) ilionesha kabumbu safi katika mchezo huo uliochezwa katika dimba la Nelson Mandela Bay nchini Afrika ya Kusini.

Zambia ndiyo walitangulia kupata goli kupitia mshambuliaji wao Comfort Seleman dakika ya 19 baada ya kutumia vizuri makosa ya walinzi wa Tanzania, na kumuinamisha nyavuni golikipa Aisha Mrisho. Hadi kipindi cha kwanza kinaisha Zambia ilikuwa mbele kwa goli 1.

Kipindi cha pili kilianza kwa Tanzania kuonesha kandanda safi na kusawazisha goli hilo kwa mkwaju wa penalti kufuatia Aisha Masaka kuchezewa madhambi ndani ya 18, na Koku Kipanga kufunga penalti hiyo na kufanya dakika 90 kuisha kwa goli 1-1.

Katika mikwaju ya penalti wanawake wa Tanzania waliibuka kidedea baada ya kufunga penalti 4 dhidi ya 3 walizopata wanawake wa Zambia.

Itakumbukwa kuwa Timu ya Tanzania U-17 ilitinga fainali kibabe baada ya kushinda dhidi ya Comoro (5-1), kufungwa na Zambia (0-1), kuifunga Afrika Kusini (6-1) kabla ya kuisambaratisha Zimbabwe (10-1). Aidha, timu hiyo inatarajiwa kuwasili nchini siku ya Jumatatu saa 7:15 usiku.

JARIDA HILI LIMETOLEWA NA
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
S.L.P 1249 DODOMA, TANZANIA
Baruapepe: cd@dodomacc.go.tz